**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA FAMASI**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUSUDIO LA KUFUTA MAJINA YA WANATAALUMA WASIO NA LESENI HAI KWENYE REJESTA

**Dodoma: Julai 28, 2023**

Baraza la Famasi ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya iliyoanzishwa kupitia Kifungu Na.3 cha Sheria ya Famasi, Sura 311. Pamoja na majukumu mengine, Baraza limepewa mamlaka ya kusajili, kusimamia na kudhibiti wanataaluma wa kada ya famasi na utendaji wao.

Kifungu Na. 22, 26 na 30 cha sheria hii kinamtaka kila mwanataaluma kuhuisha taarifa zake kwenye rejesta kabla ya tarehe 31 Disemba ya kila mwaka. Aidha, Kifungu Na. 53 kimeelekeza kuwa endapo mwanataaluma hatakuwa na leseni hai kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja (1) atakuwa amejiondoa.

Hivyo basi, Ofisi ya Msajili inawatangazia wanataaluma wote kuwa, Baraza linakusudia kuondoa kwenye rejesta majina ya wanataaluma ambao watakuwa hawajahuisha taarifa zao ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili. Orodha ya wahusika itatolewa baada ya siku hizo ili kuwajulisha umma kutopokea huduma za kitaaluma zitakazotolewa na wanataaluma hao na hatua za kisheria zitachukuliwa.

Imetolewa na;

**Elizabeth Shekalaghe**
**MSAJILI**
**BARAZA LA FAMASI**